SIMON GROUP

Plot No. 53 Mikocheni Industrial Area.
P.O.Box 71800
Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2773148 / 2700991 / 2772768
Fax: +255 22 2773142 / 2775136
sgl@umojainvestments.com

MKURUGENZI WA JIJI
06 JUN 2011

6th June, 2011.

Kwa:

Msajili wa Hazina,
S.L.P 911,
Dar Es Salaam:

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam,
S.L.P 9084,
Dar Es Salaam:

YAH: PENDEKEZO LA KUWA NA MKUTANO WA WANAHISA WA SHIRIKA LA UDA TAREHE 10 JUNI 2011

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

Kufuatia makubaliano yaliyopelekea kampuni yetu ya SIMON GROUP LTD (SGL) kununua hisa katika Shirika la Usafiri Dar Es Salaam (UDA), kwa sasa kampuni hii ni mwanahisa anayemiliki 52.535% ya hisa zote za shirika hilo hivyo kuwa na haki zote za mwanahisa kulingana na mkataba wetu wa mauziano ya hisa hizo.

Katika mkataba wetu, ibara ya 4.4.1 ilieleza kuwa katika muda usiozidi wiki mbili (siku 14) tu baada kusaini mkataba huo, ungeitishwa mkutano maalum wa wanahisa ili kufanya maamuzi katika mambo ya msingi yafuatayo

1. kutambuana kama wanahisa na kumpa mwanahisa mpya, yaani SGL nafasi ya kuendesha na kufufua shirika/kampuni
2. kupanga bodi mpya ya wakurugenzi kwa ajili ya kuendesha shirika
3. kuchagua wakaguzi (auditors) na benki wa shirika/kampuni
4. kupanga mwaka wa fedha wa shirika/kampuni

Pamoja na makubaliano hayo ya kuitisha mkutano huo katika kipindi cha wiki mbili/kisichozidi wiki mbili mara tu baada ya kusaini mkataba, tulidhani kuwa bodi ya wakurugenzi iliyopo ingesaidia katika kuitisha mkutano huo maalum na hatimaye kutufikisha katika makabidhiano ya uongozi wa shirika/kampuni katika hali ya utulivu na kuheshimiana.

Kinyume na mategemeo ya kuwa na mkutano maalum ndani ya wiki mbili, ambapo hadi leo ni jumla ya wiki 16 (siku 115), bodi hiyo kwa sababu tusizozijua sisi,haionyeshi dalili yoyote ya kutekeleza mambo ya msingi tuliyokubaliana katika mkataba na imekuwa ikiendesha vikao vya bodi na kufanya maamuzi ya mambo makubwa yanayogusa maslahi ya kampuni bila ya kushirikishwa sisi kama wawekezaji na wanahisa.

Kufuatia hali hiyo, tumechukua hatua ya kumkumbusha Meneja Mkuu wa Shirika la UDA ambaye ni Katibu wa Bodi kwa barua zetu za tarehe 25 Mei 2011 na tarehe 1 Juni 2011 ili aitishe kikao hicho lakini amebaki kimya bila maelezo yoyote ya kueleweka, hali ambayo ni ya hatari si kwa maslahi ya SGL tu kama mwekezaji bali n hatari pia kwa wanahisa wenzangu na hatma ya Shirika kwa ujumla.

Izingatiwe kuwa mazingira haya ya kutoheshimu makubaliano katika mkataba wetu inatufanya tuwe na mashaka makubwa na hata kukosa imani juu ya mambo mengine tunayopaswa kutekeleza kwa upande wetu chini ya makubaliano ya mkataba wetu, suala la kuendelea kuingiza malipo ya hisa zetu za mikupuo inayofuata likiwa mojawapo kutokana na kutokuwepo na uwazi na hofu juu ya mwenendo mzima kwa sasa unaotokana na uongozi wa Meneja Mkuu na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika.

Kwa hali hiyo, tunadhani njia pekee ya kuokoa shirika na kulinda haki zetu ni kwa wanahisa wenyewe kuingilia kati kwa kuitisha kikao maalum (extra ordinary meeting) ili kufanya maamuzi juu ya mstakabali wa shirika.

Tunapendekeza kikao cha wanahisa wote ambao ni Serikali Kuu (Msajili wa Hazina), Halmashauri ya Jiji na sisi Simon Group Ltd kikae tarehe **10 Juni 2011 saa (3) tatu Asubuhi katika ukumbi wa mikutano wa Shirika la UDA** ili tuweze kujadiliana tuliyoyaeleza.

Aidha, ieleweke kwamba kikao tunachoomba ni cha kimkataba kama kinavyoelezwa katika mkataba wetu ibara ya 4.4.1 na siyo kile cha sheria ya makampuni ambacho bila kufanya hivyo kutakuwa na uvunjifu wa mkataba huu, jambo ambalo linaweza kutufikisha katika mgogoro wa kisheria usio wa lazima.

Tunakuambatanishia nakala ya mkataba na barua husika kwa rejea ya ofisi yako

Wako,

Robert Kisena
Mwenyekiti Mtendaji



Nakala kwa:

1. Mstahiki Meya, Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam
2. Mh.Waziri wa Fedha na Uchumi
3. Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Uchumi
4. Mh. Waziri wa Uchukuzi na Usafirishaji 6/6/2011
5. Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi na Usafirishaji 6/6/2011
6. Mawakili, K & M (Advocates)

